# MIELEKEO YA UJIFUNZAJI: UCHAMBUZI WA KIMATAIFA WA MADA

Ripoti ya Kitaalamu, Februari 2023

# UTANGULIZI

**Matokeo ya utafiti uliofanywa katika miongo kadhaa iliyopita yamedhihirisha umuhimu wa watoto kulelewa au kukulia katika familia zilizo salama na zenye upendo kuliko kukulia katika taasisi. Ili watoto wanawiri maishani, hawahitaji tu afya ya kimsingi, wala lishe na usafi pekee bali wanahitaji pia malezi[1] maalum kutoka kwa mtu mzima anayeaminika - malezi ambayo taasisi, kwa namna zilivyo, haziwezi kuwapa.[2,3,4]**

Licha ya hayo, inakadiriwa kuwa watoto milioni 5.4 duniani kote wanaishi katika taasisi hizi,[5] ambazo haziwezi kutosheleza mahitaji yao mbali na kuwa huwa zinapuuza haki zao.[6] Hii inajumuisha idadi kubwa ya taasisi za kielimu ambazo, ingawa zimeundwa mahsusi kutoa elimu, zinaweza kuiga kanuni na desturi za kitaasisi ambazo ushahidi umethibitisha kuwa zinaweza kuwadhuru watoto hao.

Haki ya kila mtoto kuishi na familia yake imejikita katika mikataba kadhaa, kama vile katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watoto (CRC),[7] na Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Walemavu (CRPD).[8] Haki hii pia imefafanuliwa katika nyaraka na miongozo muhimu, ukiwemo Mwongozo wa Malezi Mbadala ya Watoto, ambao unatoa wito kwa Mataifa kuchukua hatua ili kuzuia kutenganishwa kwa watoto na familia zao kadri inavyowezekana.[9] Mkataba kuhusu Haki za Watoto, uliopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka wa 2019, unayataka Mataifa kuchukua hatua za kuzuia utenganishaji usio wa lazima wa watoto na wazazi wao.[10]

Aidha, kila mtoto ana haki ya kupata elimu: elimu ina wajibu muhimu katika ukuaji wa mtoto na katika muktadha mpana, hukuza demokrasia, amani, maendeleo na ustawi wa kiuchumi. [11] Umuhimu wake umeainishwa katika CRC, [12] na pia katika Agano la Kimataifa kuhusu Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni (ICESCR), [13] na katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR).[14] Haki ya kupata elimu, kama tu zilivyo haki nyingine zote za watoto, inawahusu watoto wote kwa usawa bila ubaguzi. CRPD inatilia mkazo hasa haki ya watoto walemavu kupata elimu sawa na watoto wengine, na kutoa wito kwa mifumo ya elimu "kuhakikisha kuna elimu-jumuishi, bora na yenye usawa kwa wote na kukuza fursa za elimu maishani mwa watu wote.[15]

**Watoto wana haki ya kukulia kwenye familia na kupata elimu bora inayokidhi mahitaji yao. Hata hivyo, matokeo ya Mpango wa Lumos yamebaini kwamba haki za watoto kupata malezi ya familia na elimu wakati mwingine zinaonekana kuzua ukinzani au hata kutojalizana. Kadhalika, tumeshuhudia pia kuwa suluhu za kibunifu, kiutendaji na za kisera zinaweza kuwawezesha watoto wote kufurahia kikamilifu haki zote mbili, ambazo ni muhimu kwa ukuaji bora.**



## MUHTASARI WA RIPOTI HII YA KITAALAMU

Ripoti hii ndiyo ya kwanza kuchapishwa kutokana na Tathmini/Uchambuzi wa Kimataifa wa Mada wa Lumos kuhusu Elimu. Inaangazia matokeo muhimu, uchanganuzi, hitimisho na mapendekezo muhimu yanayotokana na utafiti huu, ambayo yataweka msingi wa majadiliano zaidi yatakayohusisha wataalamu katika nyanja husika. Ujumbe uliomo katika ripoti hii utathibitishwa kupitia mfululizo wa majadiliano na wadau wakuu. Kwa hivyo, Lumos inakaribisha maoni na tafakari zote kuhusu matini/ujumbe huu. Kufuatia harakati hii ya uthibitishaji, ripoti kamili itachapishwa katikati ya mwaka wa 2023.

**Tafadhali wasiliana na lucy.halton@wearelumos.org ili kutoa maoni yoyote kuhusu Ripoti hii.**

## MBINU YA UTAFITI

**Utafiti huu ulifanyika mwaka wa 2021 na 2022. Unajumuisha:**

- Uchambuzi wa kitaalamu wa matini uliofanywa na Chuo Kikuu cha University College London.
- Wito wa kutoa ushahidi katika lugha nyingi (Kiingereza, Kifaransa na Kihispania).
- Majadiliano ya vikundi vya washiriki 27 kutoka nchi mbalimbali, wanaofanya kazi katika taasisi za elimu na vituo vya malezi.
- Vielelezo vinne vilibuniwa kwa kutumia data iliyokusanywa kwa mbinu zinazozingatia ubora zikijumuisha uchanganuzi wa nyaraka na mahojiano na wataalamu kwa lengo la kukusanya mitazamo kutoka nchini Colombia, Moldova, Indonesia na Umoja wa Ulaya (EU).
- Uchanganuzi wa pili wa data ya kijadi ulifanyika katika nchi tano za kusini, kati na mashariki mwa Ulaya: Jamhuri ya Czech, Moldova, Bulgaria, Ugiriki na Urusi (unaorejelewa katika ripoti hii kama 'data ya Mpango wa utafiti wa Lumos'). Nchi hizi zote ama zilikuwa katika hatua za awali zaidi au mwanzoni mwa mageuzi ya malezi, katika kipindi ambacho utafiti huu ulikuwa unafanyika kwa mara ya kwanza, kati ya mwaka wa 2012 hadi 2017.

## FASIRI YA 'MFUMO WA MALEZI YA KUISHI SHULENI/VITUO VYA

**Je, ni nini maana ya "mfumo wa malezi ya kuishi shuleni"?**
Kwa minajili ya utafiti huu, tumefafanua maana ya mfumo wa malezi ya kuishi shuleni kuwa unaojumuisha: vituo vya malezi vya mabweni, vituo vya elimu vya mabweni na vya kutwa. Kwa mantiki hiyo, tumeangazia pia uhusiano na mfanano wa huduma kati ya taasisi hizi, na muktadha mpana unaohusu mfumo huo wa malezi. Muktadha huo mpana unajumuisha hali za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni, za kihistoria/kijadi na za kisasa. Hali hizi za kimuktadha huchangia watoto kupelekwa katika vituo hivyo, na fursa za masomo ambazo wanaweza au hawawezi kupata wakiwa katika vituo hivyo.

Kwa madhumuni ya utafiti huu, tumetofautisha aina mbili za huduma za malezi yasiyokuwa ya nyumbani/makazi: vituo vya mabweni na vituo vya elimu vya mabweni. Hata ingawa vinahusiana kwa karibu, mara nyingi vikifanana kwa kiasi kikubwa, kuna tofauti baina yavyo. Katika ripoti hii vimefasiriwa hivi:

**Vituo vya malezi vya mabweni** kwa kawaida huwa sehemu ya mfumo wa mahitaji ya watoto na kimsingi huanzishwa kwa mafaa ya watoto waliobainishwa kuwa wanahitaji malezi yasiyo ya nyumbani. Aina fulani ya elimu pia inaweza kutolewa katika vituo hivi. Vinginevyo, watoto wanaoishi katika vituo hivi wanaweza kwenda shule za karibu au vituo vingine vilivyo karibu.

**Vituo vya elimu vya mabweni** huanzishwa mahsusi ili kutoa elimu, ingawa vinaweza kutoa huduma nyingine pia.

## VITUO VYA ELIMU VYA MABWENI

Vituo vya elimu vya mabweni, vikiwemo shule za mabweni, kwa kawaida havichukuliwi kuwa taasisi za 'kiasili'. Mara kwa mara huwa chini ya Wizara ya Elimu badala ya sekta ya Huduma ya Kulinda Jamii au ya Kulinda Watoto. Hata hivyo, vituo hivi vinaweza kuwa na sifa na changamoto za kitaasisi zinazofanana na vituo vya malezi vya mabweni kama vile makao ya mayatima au makao ya watoto. Mfano wa changamoto hizo ni kama vile kuwatenganisha watoto na familia au jamii zao. Matokeo ya awali ya Haki ya Kila Mtoto kuwa katika Familia yamebaini kwamba watoto katika vituo vya elimu vya mabweni (taasisi za elimu za kuishi shuleni) wanaweza kukumbana na changamoto sawa na wale walio katika vituo vya huduma za malezi.16 Hii inashadidia umuhimu wa kuelewa fasili ya 'taasisi' unapozingatia watoto waliotenganishwa na familia zao kwa kuishi katika taasisi yoyote kati ya hizi.[17]

Tofauti za kisekta na miktadha mbalimbali katika kutoa fasili/ufafanuzi kuhusu taasisi, zina maana kwamba ni vigumu kujua ni taasisi ngapi za elimu za mabweni zipo duniani kote. Kwa mfano, kuzitaja taasisi za huduma za malezi kuwa sawa na 'shule za mabweni' kunaweza kuvuruga takwimu za kitaifa kuhusu idadi ya taasisi zilizopo.[18,19] Hii inasisitiza umuhimu wa kuwepo kwa fasili bayana na kubalifu kwa wote, na umuhimu wa kuhakikisha kuwa harakati za mageuzi ya malezi zinatumia fasili pana zaidi iwezekanavyo kurejelea istilahi 'taasisi'. Kwa njia hii, aina zote za taasisi - zikiwemo taasisi za elimu za mabweni - zinaweza kusaidiwa katika harakati ya mageuzi, badala ya mageuzi hayo kujikita tu katika vituo ambavyo, katika hali ya kawaida, ndivyo hurejelewa kama taasisi (kwa mfano, makao ya mayatima).



## MSIMAMO WA LUMOS KUHUSU ELIMU YA TAASISI ZA MAKAZI/MABWENI

Lumos hujitahidi kuhakikisha kuwa watoto wote wanalelewa katika familia na wako salama dhidi ya madhara yanayojitokeza katika taasisi zinazotoa makazi ya aina yoyote ile. Taasisi inayotoa makazi ni kituo chochote cha makazi ambacho kina sifa ya kitaasisi; kwa mfano huwatenganisha watoto na familia au jamii zao, au huwa na taratibu ngumu zinazopuuza mahitaji anayotaka mtu binafsi.

Ushahidi uliojumuishwa kwenye Uchambuzi huu wa Mada unakumbatia mtazamo wa kimataifa wa elimu ya kutoa makazi/taasisi za mabweni lakini haujadili hasa madhara ya elimu maarufu ya kutoa makazi kwa ukuaji wa watoto, suala ambalo lina ushahidi haba. Hii ni kwa sababu ushahidi kama huo haukujumuishwa katika uchambuzi wa matini, na mada hiyo haikujitokeza (angalau kama mada kuu) wakati wa mahojiano na majadiliano ya vikundi, wala kwenye mpango wa utafiti wa Lumos. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba istilahi 'maradhi ya shule ya bweni' imetumika kutaja mseto wa dalili na sifa/ tabia zinazoonekana katika baadhi ya watu wazima waliosomea katika shule za mabweni tangu wakiwa na umri mdogo (utafiti huu ulilenga wanafunzi wa zamani wa shule maarufu za bweni nchini Uingereza).[20] Dalili hizi zinajumuisha matatizo ya kimapenzi na mahusiano, na matatizo ya kisaikolojia na kihisia ambayo huwaandama wanafunzi hadi ukubwani.[21]

Katika mifano mingi, harakati za ukoloni ndizo zilizoibua mtindo huu wa elimu ya makazi/mabweni ulioletwa na kutumika kutoa elimu kwa watu waliodhulumiwa, na kulazimishiwa maadili na desturi za kikoloni. Shule za bweni zilizotokana na mtindo huo zilikuwa muhimu kwa harakati za 'ustaarabishaji', ambazo zimekuwa na athari mbaya kwa jamii asilia na jamii au mataifa ya mwanzo.[22] Kwa mfano, katika Amerika ya Kusini, watoto wa kiasili katika shule za mabweni nchini Brazil, Colombia, Paraguay, Venezuela na Peru walizuiwa kuzungumza lugha zao za mama au kudhihirisha utamaduni wao kwa namna fulani, kama vile kuvaa mavazi ya kitamaduni, katika mpango wa kujaribu kuwalazimisha kufuata kanuni na maadili ya kikoloni.[23,24]Canada na Australia ni mifano ya nchi ambazo shule za malazi sasa zinatajwa kuwa aina fulani ya 'mauaji ya kimbari ya utamaduni.[25,26] Sifa ya vurugu za kikoloni katika shule nyingi za malazi lazima ziwekwe wazi ili kuelewa masuala haya. Leo hii, katika muktadha fulani, shule za malazi/mabweni zinaendelea kusababisha madhara na kukiuka haki za watoto.

Uchambuzi huu wa Mada unatambua sifa hii ya kikoloni huku ukichunguza masuala mapana kuhusu elimu ya kuishi shuleni, ili kuelewa taswira kamili ya kimataifa.



## MATOKEO MUHIMU

## VICHOCHEO VYA KUSAJILIWA KATIKA TAASISI ZA KUISHI KATIKA VITUO VYA MALEZI VYA MABWENI NA TAASISI ZA ELIMU ZA MALAZI/MABWENI

### 1 Ukosefu wa huduma za malezi yasiyohitaji makazi/mabweni, au hamu ya kunufaika kwa fursa zinazotokana na kuishi katika taasisi za malezi yenye makazi

Ingawa huenda haja ya kupata elimu ilitambuliwa kama sababu kuu ya kusajiliwa katika taasisi za elimu za mabweni, katika uchambuzi wa matini hii na mpango wa utafiti wa Lumos, sababu hii pia ilitumika, ingawa nadra, kwa vituo vya huduma za malezi zilizo na makazi/malazi. Kielelezo cha nchi ya Colombia pia kilibaini kuwa elimu ya malazi inaweza kuwa njia pekee ya watoto wengi wa vijijini kwenda shule, hasa pale ambapo shule iliyo karibu iko mbali sana hadi isiwezekane mwanafunzi kusafiri kila siku akienda na kurudi.

Shule za malazi wakati mwingine zilionekana kuwezesha - au zilitazamwa kama zinazotoa - fursa nzuri za masomo kuliko shule za kutwa. Washiriki wa vikundi vya majadiliano waliangazia dhana inayoshikiliwa na wengi kwamba watoto wanakuwa na maisha bora ya baadaye kwa kupokea elimu katika shule za malazi.

"NCHINI KENYA KWA MFANO, UTAKUTA WATU WANAWEKA ELIMU MBELE. NA NDIYO SABABU WATAAMINI KUWA NI VIZURI KUMPELEKA MTOTO KATIKA SHULE YA BWENI AU MAKAO YA WATOTO."

### 2 Umaskini

Uchambuzi wa matini uligundua umaskini kuwa sababu nyingine kuu. Mpango wa Utafiti wa Lumos uligundua kuwa umaskini na changamoto zinazohusishwa nao, kama vile makazi duni, uliongeza uwezekano wa watoto kupelekwa katika makao ya watoto au taasisi za elimu za malazi zinazosimamiwa na serikali. Katika baadhi ya matukio, wazazi waliomba kwamba watoto wao wapelekwe kwenye makao ya watoto kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kuwatunza.[27]

Dhana kwamba elimu ni chombo cha maendeleo na mabadiliko ya kijamii imekita mizizi katika jamii nyingi. Kama mshiriki mmoja wa kikundi cha majadiliano alivyobainisha;

"NI CHOMBO KINACHOHUSISHWA NA DHANA YA UMASKINI, KWAMBA ELIMU NDIYO NJIA YA KUJIONDOA KATIKA UMASKINI HUO."

Uchambuzi wa matini ulionyesha uhusiano mkubwa kati ya upatikanaji wa elimu na umaskini katika nchi zenye kipato cha kadri au cha chini, hasa katika maeneo maskini zaidi. Taasisi za elimu za malazi zilitoa, au zilionekana kutoa malezi na fursa nzuri za masomo kuliko taasisi nyinginezo. Zilikidhi baadhi ya mahitaji ya msingi ya mtoto, kwa mfano kumpa chakula, makazi, mavazi, upatikanaji wa huduma za afya, na vitabu vya shule; mahitaji ambayo familia hazingeweza kumudu.[28]

Hata hivyo, kupelekwa kwenye taasisi za makazi kunaweza pia kuhusishwa na ukosefu wa usawa katika nchi zenye kipato cha kadri,[29] na katika nchi zenye mapato ya juu, ambapo huduma za malezi au taasisi za elimu za malazi zinatoa, au zinachukuliwa kutoa, fursa nzuri zaidi za masomo na fursa za maisha bora kwa watoto kutoka katika jamii zisizojiweza au zilizotengwa.[30]

### 3 Ukosefu wa kufikia huduma-jumuishi kwa watoto walio na mahitaji maalum ya kielimu au walio na ulemavu

Watoto wako katika hatari kubwa ya kupelekwa kwenye makao ya watoto na shule za malazi iwapo upatikanaji wa elimu-jumuishi katika jamii na huduma nyingine ni nadra. Mpango wa Utafiti wa Lumos ulionyesha kwamba hii ilitokea hasa kwa watoto walio na mahitaji maalum ya kielimu au walio na ulemavu (SEND). Katika visa vingine watoto wa SEND hawakuwa na njia nyingine ila kusoma wakiwa wanaishi shuleni. Hata hivyo, kulikuwa na sababu za kijamii za kusajiliwa katika taasisi ambazo zilikuwa zikikidhi mahitaji mbalimbali zaidi ya elimu kwa watoto. Mahitaji hayo yalijumuisha malezi ya jumla, kuepushia mzigo familia ambazo tayari zilikuwa zinakabiliwa na ugumu wa kifedha au uthabiti wa kifamilia.

## 4 Kubaguliwa kwa jamii zilizotengwa na zisizojiweza

Katika hali nyingine, viongozi wa serikali huruhusu au kutetea baadhi ya makundi ya watoto kusajiliwa katika makao ya watoto kwa njia ambayo huathiri zaidi wale wanaotoka katika jamii zilizotengwa au zisizojiweza. Hii inajumuisha watoto wanaorandaranda mitaani na wale wanaotoka katika jamii au makabila ya kiasili, ambao upataji elimu unaweza kutumika kama sababu ya kushurutushwa kupelekwa katika taasisi hizo. Mshiriki wa kikundi cha majadiliano alibaini kuwa,

"MAAFISA WA POLISI, MAJAJI NA VYOMBO VINGINE MBALIMBALI VYA SERIKALI VINAPOKUTANA NA WATOTO WA KURANDARANDA, HULAZIMISHA KUONDOLEWA KWAO MITAANI NA KUPELEKWA KATIKA TAASISI HIZO, MARA NYINGI WAKITUMIA HAKI YA KUPATA ELIMU KAMA SABABU YA KUFANYA HIVYO."

Mpango wa Utafiti wa Lumos uligundua kuwa ubaguzi huu wa kitaratibu ulisababisha kutenganishwa kusiko kwa lazima kwa watoto wa Kirumi na familia zao, katika mazingira yenye huduma na usaidizi duni.[31] Umaskini na makazi duni zilikuwa sababu za kupeleka watoto wa Kirumi katika taasisi hizo. Katika nyingi ya sampuli za utafiti, watoto walikuwa wengi kupita kiasi kwenye taasisi nyingi.[32]

## 5 Sababu nyingine zilijumuisha unyanyasaji, kutelekezwa, masuala ya kitabia na/au ukiukaji wa sheria

**Sababu nyingine za kuwapeleka katika makao ya watoto na shule za malazi ni pamoja na:**

- Unyanyasaji na kutelekezwa. Mpango wa Utafiti wa Lumos uligundua kuwa unyanyasaji na utelekezaji ulisababisha watoto kupelekwa katika aina zote mbili za makazi, lakini hazikuwa hasa ndizo sababu kuu.
- Kufiwa na mlezi kulitambuliwa, katika uchambuzi wa matini, kama sababu ya kusajili watoto katika huduma za makazi kwa jumla. Kulitajwa kama sababu ya kuingizwa kwenye shule za malazi katika uchambuzi mmoja pekee wa kitaalamu wa matini.
- Masuala ya kitabia, wakati mwingine yalisababisha ukiukaji wa sheria.[33,34]
- Majanga,[35] au maradhi, katika familia.[37]
- Mazingira yenye ghasia zaidi, na ukosefu wa uthabiti katika jamii uliohusishwa na umaskini.[38]
- Hali ya mzazi aliyesomea au kukulia katika makao hayo, iliibua 'mazoea ya kujirudia kwa tatizo hilo'[39]
- Upatikanaji wa elimu ya kidini, kama vile madrasa.[40]



# ATHARI YA TAASISI ZA MAKAZI KWA ELIMU NA MAISHA YA MTOTO

UTAFITI HUU ULIFICHUA KUWA ATHARI ZA MALEZI YA KUISHI MBALI NA NYUMBANI, NA SHULE ZA MAKAZI KWA MATOKEO YA WATOTO ZILIKUWA CHANGAMANO. KWAMBA TAASISI HIZO ZINAWEZA KUCHANGIA KUONGEZEKA AU KUPUNGUA KWA ATHARI HIZO KWENYE HALI ASILIA YA MTOTO.

### 1. Kuhudhuria masomo shuleni & upatikanaji wa elimu

Taasisi za kielimu za makazi shuleni na vituo vya makazi ya watoto vilidhihirika kuzidisha upatikanaji wa elimu na nafasi za masomo ambazo zinaweza kufaidi watoto na familia zao.[41] Hata hivyo, hali haikuwa hivyo nyakati zote. Kwa mfano, mpango wa utafiti wa Lumos uligundua kuwa baadhi ya watoto katika makazi ya watoto - yanayotoa elimu humo ndani na yale yasiyotoa - walikosa elimu kabisa. Watoto walemavu au wale ambao tabia zao ni tata ndio walio katika hatari kubwa ya kuathirika; katika taasisi moja iliyotoa elimu, 46% ya watoto hawakuwa wakipata elimu.

### 2. Maendeleo ya kielimu na uhusiano shuleni

Utafiti huu ulionyesha mseto wa matokeo chanya/mazuri [42] na hasi/mabaya[43] kuhusu maendeleo ya kielimu na uhusiano shuleni, kwa watoto wanaoishi katika makao ya watoto na taasisi za kielimu za malazi. Wakati mwingine, matokeo chanya na hasi yalijiri kwa pamoja.

Baadhi ya tafiti ziligundua uwepo wa matokeo bora ya kiakademia kwa baadhi ya watu, wakiwemo watoto wanaoishi katika umaskini mkubwa au kutoka katika makundi ya watu wasiojiweza au waliotengwa tangu jadi.[44] Hata hivyo, matokeo pungufu ya kiakademia yaliyozoeleka pamoja na changamoto za ugumu wa kuzoea hali au maisha mapya, yalishuhudiwa katika aina zote mbili za makazi ya watoto.[45,46,47,48] Katika makao ya watoto, mazoea ya kutumia mbinu moja ya matibabu kwa walemavu, ambayo huzingatia ulemevu wa mtoto na ukosefu wake wa uwezo, iligunduliwa kudhoofisha uwezo wa kujifunza wa watoto.[49]

### 3. Matokeo ya afya na ustawi

Tafiti za uchambuzi wa matini zilizochunguza matokeo ya afya na ustawi kwa watoto walio katika taasisi za kielimu za malazi zilibaini matokeo chanya [50] na hasi[51] yanayohusiana na afya ya kimwili na ustawi wa kiakili, kijamii na kihisia kwa watoto.

Zilibaini kuwa uhusiano wa kifamilia uliovurugika pamoja na kuhamishwa kwa mtoto kutoka nyumbani kwao, unaweza kuwa na athari mbaya ijapo katika suala la ujitambulishaji wa mtoto, ukuaji wake wa kihisia na afya ya akili ya mtoto huyo.[52]

### 4. Usalama wa watoto katika taasisi za kielimu za malazi/makazi[53]

Tafiti tatu pekee katika uchambuzi wa matini ndizo zilijadili matokeo yanayohusiana na usalama, na mtoto kusukumwa katika aina mbalimbali za madhara.[54] Zote tatu zilitaja tu matokeo mabaya ya kiusalama na madhara yanayohusiana nayo, ukiwemo ukandamizaji wa watoto, ongezeko la ajira kwa watoto, unyanyasaji wa kimwili, kingono na matusi na aina nyinginezo za dhuluma.[55]

## JINSI SERA NA DESTURI ZINAVYOWEZA KUCHANGIA UPATIKANAJI WA HAKI ZA WATOTO ZA KUPATA ELIMU NA MAISHA YA KIFAMILIA

**1. Mwongozo wa kisheria na kiserikali ni muhimu katika kuhakikisha watoto wote wanapata elimu bila kuishi shuleni**
Kielelezo cha nchini Moldova (tazama hapa chini, ukurasa wa 10) kinaonyesha umuhimu wa kuwa na miongozo muhimu ya kisheria na kiserikali ili kuhakikisha kwamba watoto wanapata elimu bila kuishi shuleni na huduma nyingine zinazokidhi mahitaji yao.

**2. Mbinu ya sekta-mseto ya kushirikisha 'mfumo mzima', inayotumiwa katika ngazi zote baina ya serikali na familia, inaweza kusaidia kushughulikia vichocheo vikuu vya kijamii na kielimu vya kusajili watoto katika taasisi za malazi**
Kielelezo cha nchini Moldova (tazama hapa chini - uk 10) kinabaini kuwa kila mara elimu ya malazi ilitajwa na serikali kama mwelekeo muhimu wa ajenda pana ya mageuzi katika malezi, ikishirikishwa na wizara ya Elimu na ile ya Huduma na Afya ya Jamii. Nchi hii inaonyesha kuwa mbinu ya ushirikiano wa sekta-mseto katika mageuzi haya ya malezi inaweza kuhakikisha kuwa taasisi zilizo chini ya sekta hizo mbalimbali zinahusishwa katika mageuzi hayo.

Uchambuzi huo wa matini ulibaini kuwa mbinu ya sekta-mseto katika utoaji wa huduma na usaidizi wa familia inaweza kuibua matokeo ya jumla kuhusu vichocheo mbalimbali vya kijamii na kiuchumi ambavyo vinachangia watoto kupelekwa katika makao ya watoto.[56]

**3. Madhara kwa ukuaji yanayosababishwa na elimu ya malazi hayawezi kuzuiwa ipasavyo, ama kwa juhudi za kushughulikia vipengele mahsusi vya kitaasisi au kwa kuboresha matokeo ya watoto kwa namna nyinginezo.**
Baadhi ya tafiti kwenye uchambuzi wa matini zilibaini suluhu zilizoleta matokeo chanya (mazuri), kama vile sifa nzuri za kielimu,[57] au utoaji bora wa elimu.[58] Hata hivyo, nyingine ziligundua kuwa watoto wengi wanaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali, kama vile matatizo ya ukuaji wa kihisia na kitabia,[59] au matokeo ya kielimu kudorora,[60] licha ya kuwepo kwa suluhu zilizobuniwa ili kuyaboresha.



## COLOMBIA

**Sera na taratibu ya elimu ndivyo vichocheo vya watoto kupelekwa katika taasisi hizi.** Elimu ya malazi ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kuwezesha watoto kupata elimu katika maeneo ya vijijini na mashambani, ambako kwa watoto wengi shule hazipo karibu na nyumbani.[61] Ukosefu wa elimu katika jamii za vijijini wanakotoka watoto ulikuwa sababu kuu ya watoto kujiunga na elimu ya malazi.

**Sababu za kijamii za kujisajili katika taasisi, kwa mfano upatikanaji wa chakula au malezi ya watoto wakati wazazi wao wameenda kazini, pia zilikuwa nyingi,** hali inayoweza kutoa sababu ya watoto wanaoishi karibu zaidi pia kuenda shule za bweni. Kulikuwa na idadi kubwa kupita kiasi ya wanafunzi kutoka katika makabila madogo madogo, hasa wale wanaotoka katika jamii za kiasili, ambapo kulikuwa na uwezekano mdogo wa wao kuwasiliana mara kwa mara na familia zao na uwezekano mkubwa wa kuhudhuria masomo yaliyokusudiwa kwa watoto wadogo.

**Elimu ya malazi inaweza kuwawezesha na kuwazuia watoto kupata haki zao zote kikamilifu.** Ingawa watoto wanapata haki yao ya elimu, wananyimwa haki yao ya kukulia kwenye familia. Haki zote mbili zimebainishwa katika sheria za Colombia, na pia katika mikataba na miongozo ya kimataifa. Kutenganishwa kwa watoto na familia zao ili kuhudhuria masomo - mara nyingi wakiwa mbali zaidi, na miundomsingi duni ya mawasiliano – hutatiza sana familia nyingi kutekeleza sehemu muhimu katika maisha ya kila siku ya watoto wao.

**Haki ya watoto kuwa salama na kupata ulinzi inahujumiwa** na mazingira yaliyo ndani ya shule na ukosefu wa mifumo bora ya usalama, na kwa kutenganishwa kwao na huduma za afya na ulinzi zilizo nje ya taasisi hiyo.

## UMOJA WA ULAYA[62] 6

**Umoja wa Ulaya umeonyesha jinsi mbinu za ufadhili zinavyoweza kutumika kitaalamu kuvumisha mageuzi ya malezi na elimu-jumuishi.** Juhudi hizi zimepata nguvu kutokana na kujumuishwa kwa mageuzi ya malezi na elimu-jumuishi katika sera za Umoja wa Ulaya kuhusu haki za kimsingi za binadamu.

**Hata hivyo, ulingano bayana zaidi kati ya mageuzi ya malezi na elimu-jumuishi katika ngazi ya sera au mipango, inaweza kuimarisha mafanikio haya.** Kwa kuzingatia ulingano wa kiasilia kati ya mambo haya mawili, mbinu jumuishi zaidi inaweza kuchochea kuibuka kwa athari nyingi kwani mageuzi yanayopatikana katika kila nyanja yanaweza kuchangizana, kuingiliana na kuimarishana.

## MOLDOVA

**Pakiwepo usaidizi unaofaa, watoto walio na mahitaji maalum na walemavu wanaweza kujifunza katika mazingira rasmi ya elimu.** Ukuzaji wa elimu-jumuishi nchini Moldova umeondoa dhana miongoni mwa baadhi ya watu kwamba kuanzishwa kwa taasisi za makazi shuleni kwa watoto wenye ulemavu ni "lazima".

**Mbinu ya kimfumo na shirikishi ya sekta mbalimbali inayohusisha mashirika ya umma kutoka katika sekta ya elimu na huduma ya kulinda jamii na wadau wakuu kama vile Mashirika Yasiyo ya Serikali**, imeimarisha mafanikio ya Moldova kuleta mageuzi katika mfumo wa malezi ya watoto na kuendeleza elimu-jumuishi katika harakati ya mageuzi ya malezi. Mbinu hii inabaini kwamba mageuzi ya malezi na ya elimu yanaenda bega kwa bega, yanaingiliana na - kwa kiwango kikubwa – ni viungo muhimu visivyotenganishwa katika harakati ya jumla ya mageuzi ya malezi ya watoto.

**Sheria na sera**, kuanzia kwa mkakati mkuu wa kitaifa na mpango-kazi wa mageuzi ya malezi, zinazojumuisha sekta ya elimu, huduma za kulinda jamii, na afya, hadi kwa vipengee mahsusi zaidi vikiwemo miongozo ya dhana na sheria kuhusu elimu-jumuishi, zimepunguza sana idadi ya watoto wanaojipa elimu ya malazi na aina nyinginezo za taratibu za kitaasisi, na kuongeza idadi ya watoto wenye SEND katika shule rasmi zisizo za bweni.

**Utekelezaji na ufuatiliaji usiokoma unahitajika** huku Moldova ikiendelea kutekeleza mageuzi.

**Ushiriki wa wafadhili katika kubuni huduma-jumuishi ni muhimu sana** kwani umeongeza thamani katika mchango wa serikali.

## INDONESIA

**Walezi katika makao ya watoto, walio na mafunzo faafu na wanaoweza kukuza uwezo, wametumwa upya** kuhudumu kama wakufunzi wanaoishi na jamii husika, pamoja na wahudumu wa malezi ya kutwa/ nyumbani kwa watoto wenye ulemavu wa wastani na mkubwa.

**Mbinu ya sekta-mseto imefaulisha utumaji huu wa walezi kutekeleza majukumu ambayo kwa kawaida huwa chini ya sekta tofauti.** Uhamisho wa wafanyakazi kutoka katika huduma ya malezi hadi ya elimu unamaanisha kuwa wafanyakazi hao wanaweza kutumwa mahali wanapohitajika, na pia umefungua nafasi za mafunzo na maendeleo ya kitaaluma.

**Kuziwezesha na kuimarisha familia ili zisaidie na kuchangia katika elimu ya watoto wao** kumehakikisha kuwa watoto walemavu hawanyimwi elimu.

**Ushiriki wa watoto katika elimu inayotolewa katika jamii umesaidia kubadilisha mitazamo** katika familia na jamii kuhusu kuelimisha watoto walemavu, na kuondoa vikwazo vya ushirikishaji wa kila mtu.



## HITIMISHO NA MIJADALA MUHIMU

**Katika sehemu nyingi duniani, familia zinalazimika kuchagua moja kati ya haki za kimsingi za watoto wao: haki ya kupata elimu, na haki ya kukulia katika familia.** Haki zote hizo za watoto haziwezi kugawika kwa kuwa zinashabihiana: haki ya kupata elimu na haki ya kukulia katika familia zinafaa kueleweka kuwa zinatoshana kwa umuhimu na zinachangiana, nazo serikali zinafaa kuhakikisha kuwa familia zote katika jamii zinapata huduma bora ili kuziwezesha jamii hizo pamoja na watoto wao kufanya maamuzi huru na sahihi kuhusu elimu. Elimu ya kuishi shuleni inaweza kutoa, au kutazamwa kama inayotoa fursa nzuri zaidi, lakini hii bila shaka ina 'gharama' yake; kutenganisha watoto na familia zao.

**Upatikanaji wa elimu-jumuishi na bora zaidi katika jamii ni muhimu katika kufanikisha mageuzi ya malezi.** Kimsingi, mageuzi katika sekta ya elimu na huduma za kulinda jamii yanapaswa kufanywa kwa pamoja, kwa kutumia mbinu ya mfumo-mzima pamoja na upangaji na ushirikiano kati ya sekta hizi mbili na nyinginezo.

**Udhaifu wa kijamii na kiuchumi huongeza hatari ya utenganishi usio wa lazima wa watoto na familia zao, na huchochea watoto kujiunga na taasisi za elimu ya shule za malazi.** Utafiti huu ulibaini kuwa watoto wanakubaliwa kujiunga na taasisi za malezi iwapo wazazi hawana njia au uwezo wa kuwatunza. Hii inatilia mkazo haja ya kushughulikia sababu za kijamii za kujiunga na taasisi hizi kupitia kwa huduma na usaidizi unatolewa katika jamii, unaoweza kuwafikia watoto na familia zote zinazouhitaji.

**Kuwa katika elimu ya malazi kunadhuru afya, ustawi na ukuaji wa watoto, sawa tu na kunavyowadhuru katika taasisi za makazi.** Ni wazi pia kwamba dhana fulani - kama vile imani kwamba kupokea elimu ya malazi bila shaka kutasababisha matokeo bora ya kielimu- aghalabu hazina msingi. Utafiti huu unaonyesha kuwa ingawa baadhi ya matokeo chanya/mazuri yanaweza kutokea kwa baadhi ya watoto, matokeo haya yanaweza kuandamana na kuvurugwa na athari nyingine hasi.

**Kuelewa na kushughulikia kanuni, mitazamo na mazoea ni zana muhimu ya kuleta mabadiliko.** Ni muhimu kuelewa na kushughulikia jinsi mambo haya yanavyoweza kuathiri maamuzi ya kuwapeleka watoto katika taasisi za malezi, na wakati mwingine kuakisi ubaguzi kwa makundi yaliyotengwa.

**Harakati za mageuzi zinafaa kuhusisha sekta ya huduma ya kutunza jamii na ile ya elimu, pamoja na mipangilio na ushirikiano wa pamoja,** ili kuwezesha mbinu jumuishi ya mageuzi elimu na malezi. Hili ni muhimu katika kushughulikia sababu mbalimbali za kujiunga na taasisi hizi katika jamii, na kuhakikisha kuwa juhudi za sekta mbalimbali zinajalizana.

**Suluhu za sekta-mseto ni njia nzuri ya kuwezesha uhamishaji mzuri wa rasilimali kutoka taasisi za makazi hadi zisizo za makazi, na baina ya sekta mbalimbali inapohitajika.[63]** Hii inajumuisha wafanyakazi (nguvukazi), rasilimali za kifedha na nyenzo. Huduma za makazi mara nyingi ni ghali mno kuzimudu, ikilinganishwa na zile zisizo za makazi, kumaanisha kuwa rasilimali muhimu za kifedha zinaweza kutumika kusaidia idadi kubwa ya watoto katika jamii kuliko katika taasisi za makazi.[64] **Hii ina manufaa ya kuepuka madhara ya kitaasisi huku ikielekeza rasilimali zaidi katika kuzuia utenganishaji usio wa lazima.**

Hata ikiwa suluhu za kitaasisi za makazi zinaweza kuleta matokeo chanya, zinahitaji bajeti, na wataalamu, ambazo vinginevyo zinaweza kufadhili shule za msingi katika jamii na huduma nyinginezo zinazokidhi maslahi muhimu ya watoto na kuwawezesha kupata haki zao.

**Wafadhili hutekeleza jukumu muhimu katika kuwezesha mageuzi ya malezi**, ambayo yanapaswa kuimarishwa na kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa mipango ya mageuzi ya malezi kwa jumla. Athari chanya za wafadhili wanaoelekeza rasilimali zao katika mageuzi ya malezi zinaweza kuimarishwa zaidi kwa kutambua uhusiano kati ya mageuzi ya malezi na ya kielimu, na kuhakikisha kuwa fedha zimetengwa kulingana na kusudi hilo.

**Hivi sasa hakuna utafiti mzuri uliofanya kubaini uhusiano kati ya elimu na malezi kwa kiwango cha kimataifa.** Tafiti zilizopo zinaonyesha upendeleo wa kijiografia kuelekea kaskazini mwa ulimwengu, kumaanisha kwamba uelewa wetu wa uhusiano kati ya elimu na malezi yasiyo ya nyumbani unasababishwa na istilahi, dhana, lugha na imani zinazoakisi upeo huu mdogo. Taasisi za malezi zimeundwa na kufasiriwa na istilahi za kiutawala na kisheria za mifumo ya ustawi wa kijamii katika nchi mbalimbali. Aidha, mambo mengine yanayoathiri jinsi mahitaji ya kimsingi ya watoto yanavyotimizwa na haki zao kulindwa yanafaa kutafitiwa na kufasiriwa. Kwa hivyo, ushahidi zaidi wa kimataifa unahitajika ili kuelewa kikamilifu mwingiliano kati ya malezi na elimu ya malazi.

**Pia kuna ukosefu wa takwimu kuhusu athari linganishi za matokeo ya kielimu (na gharama) kwa mtoto anayepokea elimu-jumuishi kabisa ya kutwa na mtoto anayepokea elimu ya malazi.** Vilevile, kuna pengo kubwa la matokeo ya utafiti unaohusu watoto kuhusiana na ushahidi huu, pengo ambalo linapaswa kushughulikiwa.

# MAPENDEKEZO MUHIMU YA MASHAURIANO

## KWA SERIKALI YA KITAIFA NA ZA MITAA

Serikali zinafaa kuhakikisha kwamba juhudi za kuendeleza mageuzi ya malezi na upatikanaji wa elimu zinachangiana. Mageuzi ya malezi yanapaswa kuzingatia vichocheo na masuala ya kawaida na wakati huo huo yafuate vigezo mahususi vya kimuktadha. Kwa hivyo, juhudi zote zibuniwe mahsusi kuingiliana na muktadha wa kila nchi binafsi. Mbali na hilo, mapendekezo mbalimbali yafuatayo yanafaa.

